# SOUTH EASTERN KENYA UNIVERSITY

## UNIVERSITY EXAMINATIONS 2016/2017

### FIRST YEAR EXAMINATIONS FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

### CKS 203: PHONETICS AND KISWAHILI PHONOLOGY

**DATE: 8TH DECEMBER, 2016** **TIME: 4.00-6.00PM**

**MAAGIZO**:

JIBU MASWALI **MATATU**, SWALI LA **KWANZA** NI LA **LAZIMA**

1. a) Kwa kutumia mchoro, onyesha ala mbalimbali zinazoshiriki katika utamkaji wa foni na dhima yake katika mchakakato mzima wa utolewaji wa foni.

   b) Ainisha foni zote za Kiswahili kwa kurejelea:

   i) Namna ya kutamka sauti

   ii) Ughuna wa sauti

   iii) Ung'ong'o wa sauti

   (alama 30)

2. 'Ingawa fonetiki na fonolojia hujishughulisha na uchanganuzi wa sauti za lugha, kila taaluma ina mwelekeo wake tofauti katika uchambuzi na uchunguzi'. Thibitisha.

   (alama 20)

3. Changanua sifa bainifu za fonimu zifuatazo:

   a) Irabu za juu

   b) Nazali

   c) Viyeyushi

   d) Vizuiwa kwamiza

   e) Vifyonzo

   f) Vizuiwa vya ufizi

   (alama 20)

4. a) Eleza maana ya silabi

   b) Fafanua maumbo manane ya silabi ya Kiswahili sanifu

c) Eleza muundo wa ndani wa silabi katika maneno yafuatayo kwa kutumia michoro ya matagaa

i) maua

ii) mtu

iii) labda

(alama20)

5. Huku ukitolea mifano, fafanua dhana zifuatazo kama zinavyodhihirika katika fonolojia arudhi
   a) Mkazo
   b) Kiimbo
   c) Toni
   d) Wakaa
   e) Kidatu

(alama 20)

6. Eleza kwa tafsili mifanyiko ifuatayo ya kifonolojia
   a. Udondoshaji
   b. Ukaakaishaji
   c. Kuimarika kwa fonimu
   d. Unazalishaji wa irabu
   e. Uyeyushaji

(alama 20)